

imbayo  
cupinga  
Chama  
le cha  
misingi  
iadamu  
iwafikia

waasisi  
zingatia  
'a kuwa  
tawi wa  
Rukwa,  
shukuru  
ti taarifa  
enyekiti

i Maufi,  
i kubwa  
endelea  
ukijenga

Cha  
ma,  
Ikall  
ya  
Dk.  
juzi  
kali  
chi,  
naji  
anl  
eka  
ani



## Mikakati yaanikwa uuzaaji samaki nje

### Na MWANDISHI WETU

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe, amesema wizara yake itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuhakikisha sekta ya uvuvi inakua kwa kuboresha milao ya samaki.

Lengo ni kupata samaki bora zaldi na kuongeza masoko ndani na nje ya nchi. Profesa Shemdoe alibainisha hayo jijini Dodoma juzi, kando ya kikao chake na wakurugenzi wa halmashauri ya maji, manispaa na wilaya zenye shughuli za uvuvi cha kuweka mikakati kufanikisha shughuli hiyo kuwa endelevu.

Alisema kutokana na maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aliyatoa hivi karibuni jijini Mwanza alipokuwa alikabidhi boti za uvuvi na vizimba kwa kultaka wizara hiyo kushirikiana na TAMISEMI kukuza uvuvi, maelekezo hayo yameanza kufanyiwa kazl. "Leo (juzi) tumekaa kutekeleza

“

**Leo (juzi) tumekaa  
kutekeleza maelekezo  
ambayo Rais Dk. Samia  
aliyatoa na tumepata  
wasaa kuzungumza  
na wakurugenzi wa  
halmashauri na kupanga  
mipango kuhusu namna  
bora ya kuimarisha  
maeneo ya kupokea  
samaki.**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe.

maelekezo ambayo Rais Dk. Samia aliyatoa na tumepata wasaa kuzungumza na wakurugenzi wa halmashauri na kupanga mipango kuhusu namna bora ya kuimarisha maeneo ya kupokea samaki," alisema.

Allongeza baada ya kikao hicho kutakuwa na matokeo chanya yakilwemo ya kapatikana bidhaa bora za samaki amba watakuwa wanahitajika zaldi katika viwanda ya kuchakata minofu ya samaki hatua ambayo itafungua masoko zaldi ndani na nje ya nchi.

Awali akifungua kikao hicho, Kalmu Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madalla anayeshughullika uvuvi, alisema sekta hiyo imekuwa moja ya chanzo muhimu cha mapato kwa halmashauri na taifa.

Allongeza kutokana na sekta hiyo kuwa muhimu, viwanda ya kuchakata minofu ya samaki vimekuwa vlikhitaji samaki kwa wingi kuchakata na kusafirisha minofu ya samaki katika masoko ya nje ya nchi ambayo yanaliingiza taifa fedha za kigeni.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho walisema sekta ya uvuvi ni muhimu katika halmashauri wanazotoka kwa kuwa imekuwa ikichangia kiasi kikubwa upatikanaji wa ajira.

Wizara hiyo inaendelea kukutana na wadau mbalimbali kutokana na maono ya Rais Samia ya kutaka sekta hiyo Irasimishwe kutoa fursa kwa wananchi wanaofanya shughuli hiyo kutambulika rasmi na kunufaika kuptita taasli za kifedha.

President Samia Suluhu Hassan, who spoke at the Tanzania Tannazite stadium in Babati on October 14 last year at the peak of the freedom torch race, said the nutritional situation is still not satisfactory where stunting in children under five years old at national level was 30 percent and Manyara Region is 32 percent.

Pina Vyasli (L), Director General of India's ES Healthcare Ltd, briefs journalists at the Tanzania Investment Centre (TIC) offices in Dar es Salaam yesterday to invest in Mwanza city's Tanzanite Hospital. Next to her is the hospital's Vice Chairman, Jared Awando, followed by TIC's Director of Investment Promotion, John Mnali. Photo Correspondent Joseph Mwendapole

THE GUARDIAN Pg 1.

# \*Lake Nyasa fishermen want better fishing tools \*

By Guardian Correspondent,  
Kigoma

FISHERMEN in Lake Nyasa in Kigoma District, Mbeya Region have expressed fear over the use of poor fishing tools including canoes, which puts their lives at risk when the lake gets stormy.

The fishermen raised the outcry before Kigoma District Commissioner Josephine Manase when she visited the Bombe village to inspect development

activities.

The fishermen told the DC that their lives were in danger due to the poor tools they use to carry out their fishing activities.

J

Jonathan Mwangunda who is a fisherman in Lake Nyasa said the natural canoes used by the majority of the fishermen cannot withstand the big waves caused by strong storms when the lake is disturbed.

"Many fishermen use natural canoes to go fishing in the

middle of the lake, now when strong winds blow and cause big waves, we are at great risk of drowning in the lake due to our boats not being able to withstand the waves," said Mwangunda.

He asked the government to help them with better fishing tools including canoes and modern nets so that they can do their activities productively and in a safe environment.

"Our fishing is very old-fashioned, we ask the government

to first help us teach us modern methods of fishing and also empower us by providing us with the best tools so that we can do our fishing activities productively," said Mwangunda.

On his part, Nelson Mwakilambo who is also a fisherman in the lake said that the fishing they do in Lake Nyasa was aimed at enabling them to make a living and not to bring them development.

The methods we use to catch fish allow us to get fish to sup-

port our lives, but we cannot get rid of poverty because we do not get many catches due to poor technology and the tools we use are very poor," said Mwakilambo.

Matema Ward Councillor, Antony Mwangunda said it is important for the government to empower the fishermen because they have the same rights as other Tanzanians.

Responding to the fishermen's arguments, the DC said the government has started

making efforts to empower fishermen in various areas of the country and asked the fishermen of the lake to be patient claiming that the government will reach them.

He said that the government recently provided a boat that was contested by fishermen and one of them was lucky to get it and now he is doing his activities using the modern boat. He said that President Samia Suluhu Hassan has also started distributing modern boats to

fishermen in various parts of the country and claimed that the fishermen of Lake Nyasa are also on the President's schedule saying they should wait.

"I think you have witnessed recently that the President has started distributing modern boats to fishermen and the other day we saw her doing that in Mwanza, the fishermen of our lake and they are on the schedule to be given those boats when the time comes they will be given them," she said.

habari, baada ya kukabidhi vifaa vya kufanya usafi kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya jana. Kulla ni MKUUNGENZI wa Jiji hilo, John Nchimbi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

NIPASHE UK 16

# Wavuvi Ziwa Nyasa wahofia maisha yao

Na Nebart Msokwa, KYELA

WAVUVI wanaofanya shughuli ndani ya Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya wamesema maisha yao yako hatarini kutokana na kutumia zana duni za uvuvi ikiwemo mitumbwi ya asili.

Wavuvi hao wametoa kilio hicho mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase alipotemebelea Kijiji cha Ikombe kwa ajili ya kukagua shughuli za maendeleo.

Wakizungumza kwenye fukwe za Ziwa Nyasa, baadhi ya wavuvi walisema maisha yao yako hatarini kutokana na zana duni wanazotumia kufanya shuguli zao za uvuvi.

Jonathan Mwamgunda ambaye ni mvuvi wa samaki ndani ya Ziwa Nyasa alisema

mitumbwi ya asili wanayoitumia wavuvi wengi haiwezi kuhimili mawimbi makubwa yanayosababishwa na dhoruba kali pale ziwa hilo linapochafuka.

"Wavuvi wengi tunatumia mitumbwi ya asili kwenda kuvua samaki katikati ya ziwa, sasa upepo mkali unapovuma na kusababisha mawimbi makubwa, huwa tunakuwa kwenye hatari kubwa ya kuzama ziwani kutokana na mitumbi yetu kushindwa kuhi-mili mawimbi hayo," alisema Mwamgunda.

Aliiomba serikali kuwasaidia zana bora za uvuvi ikiwemo mitumbwi na nyavu za kisasa ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija na wakiwa katika mazingira salama.

"Uvuvi wetu ni wa kizam-

ani sana, tunaiomba serikali kwanza itusaidie kutufundi-sha mbinu za kisasa za kuvua samaki na pia ituwezeshe kwa kutupatia zana bora ili tuweze kufanya shughuli zetu za uvuvi kwa tija," alisema Mwamgunda.

Kwa upande wake Nelson Mwakilambo ambaye pia ni mvuvi ndani ya ziwa hilo alisema kuwa uvuvi wanaoufanya ndani ya Ziwa Nyasa ni ule wa kuwawezesha kujikimu na sio kuwaletea maendeleo.

"Mbinu tunazozitumia kuvua samaki zinatuwezesha kupata samaki wa kujikimu tu maisha yetu, lakini hatu-wezi kujikwamua kiuchumi kwa sababu hatupati samaki wengi kutokana na teknolojia pamoja na zana zetu tunazotumia ni duni mno," alisema

Mwakilambo.

Diwani wa Kata ya Matema, Antony Mwamgunda alisema kuna umuhimu wa serikali kuwawezesha wavuvi wa ziwa hilo kwa kuwa na wao wanayo haki kama ilivyoo kwa Watanzania wengine.

Akijibu hoja za wavuvi hao, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase alisema serikali imeshaanza kufanya jithada za kuwawezesha wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini na kuwataka wavuvi hao wavute subira akidai kuwa serikali itawafikia.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameshaanza kugawa boti za kisasa kwa wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini na kusema kuwa wavuvi wa Ziwa Nyasa nao wako kwenye ratiba ya mgawo.